**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**BARAZA LA MITHANI LA TANZANIA**

**MTIHANI WA KUHITIMU KIDATO CHA SITA**

**121/1** **KISWAHILI 1**

(Kwa watahiniwa walioko na wasiokuwepo Shuleni)

**Muda: Saa 3** **ANSWERS** **Mwaka: 2022.**

**Maelekezo**

1. Karatasi hii inasehemu A na B zenye jumla ya maswali **nane (8)**
2. Jibu maswali yote katika sehemu A na maswali matatu kutoka sehemu B. Swali la tano ni la Lazima
3. Sehem A ina alama 40 na sehemu Bina alama 60
4. Zingatia maelekezo ya kila swali.

maktaba.tetea.org
TETEA



Find this and other free resources at: http://maktaba.tetea.org

*Prepared by: Maria Marco for TETEA*

1. Soma kifungu cha habari kifuatacho kwa makini kisha jibu maswali yafuatayo:

Uhuru ni ua lisilonyauka, lenye umbo zuri linalotia kiumbe yote furaha. Kasuku akinyimwa uhuru huweza kusahau ufundi wake wa kuimba, hudhoofika na hatimaye hufa kwa kihoro. Hali kadhalika, mtoto mchanga hupiga mateke na kulia anapofunganishwa, anapovishwa nguo na hata anapolishwa, hayo yote huyafanyia ilmradi tu aachwe huru.

Katika nchi yenye demokrasia mtu binafsi anayo haki ya kuishi bila kubughudhiwa au kunyanyaswa kwa namna yoyote na mtu, kikundi cha watu au serikali. Mtu ana uhuru wa kwenda popote ilimradi asivunje sheria au kuingilia uhuru wa mtu mwingine. Mtu ana uhuru wa kushiriki katika majadiliano na kutoa maamuzi ya mambo yanayoihusu mustakabali wa nchi au anaweza kuwawakilisha katika majadiliano na utoaji wa maamuzi hayo na wananchi wenzake. Mwananchi anao uhuru wa kufanya mawasiliano yoyote halali ilimradi hatoi matamko ya kuchochea au ushawishi kwa watu. Mawasiliano hayo yasiyo na hali ya uchochezi na ushawishi yasiwe yanayosababisha watu kwenda kinyume na matakwa ya uongozi. Mazungumzo yoyote yanayovuka hapo yanapasa kuchunguzwa kwa makini na mamlaka.

Katika nchi yenye demokrasia ya kweli, serikali hufanya jukumu la kulinda utu na raia wake. Aidha, serikali hutoa elimu kwa watu wake ili kuwajengea misingi bora ya kujitengenezea itakayowawezesha kujenga uchumi. Serikali ikisimamia misingi ya utawala bora wananchi huwa tayari kuhudumia taifa lao kwa moyo wote bila kinyongo kwa sababu juhudi za serikali zinaonekana.

Serikali yoyote yenye kujali utu wa raia wake, husimamia misingi ya demokrasia na haki za binadamu hivyo raia wake huishi kwa amani na ndipo maana halisi ya uhuru inapojiidhihirisha. Uhuru ni kitu chenye thamani ambacho hakiwezi kufananishwa na rangi ya nguo, wala ladha ya chakula na hakuna kitu chochote ulimwenguni kinachoweza kuwa na thamani inayoweza kufananishwa na uhuru.

Maswali:
(a) Andika kichwa cha habari kisichozidi maneno matatu.
Thamani ya Uhuru

(b) Orodhesha mawazo makuu matatu yanayopatikana katika aya ya pili.
(i) Mtu binafsi ana haki ya kuishi bila kunyanyaswa au kubughudhiwa.
(ii) Mwananchi ana uhuru wa kushiriki katika majadiliano na kutoa maamuzi yanayoihusu nchi.
(iii) Mawasiliano yasiyo ya kuchochea au ya kuingilia uhuru wa wengine yanaruhusiwa.

(c) Taja faida moja ya serikali kusimamia utawala bora.
Hukuza amani na utulivu miongoni mwa wananchi.

(d) Eleza maana ya maneno yafuatayo kama yalivyotumika katika kifungu cha habari:
(i) Kihoro: Hali ya maumivu makali ya kihisia yanayosababisha kushuka moyo au kupoteza uhai.
(ii) Demokrasia: Mfumo wa utawala unaowapa watu haki ya kushiriki katika maamuzi ya mambo ya nchi.
(iii) Kutaharuki: Hali ya mshtuko au kuchanganyikiwa.


Find this and other free resources at: http://maktaba.tetea.org

***Prepared by: Maria Marco for TETEA***

(iv) Kinyongo: Hisia ya kukasirishwa au kutoridhika na hali fulani.

2. Eleza mambo muhimu matano yanayoweza kumsaidia mtumiaji wa lugha kuwa mahiri.

(i) Kusoma vitabu mbalimbali: Kusoma huongeza msamiati, uelewa wa sarufi, na matumizi sahihi ya lugha.
(ii) Mazoezi ya kuandika: Kuandika mara kwa mara husaidia mtumiaji wa lugha kuboresha ufasaha na ubunifu.
(iii) Mazungumzo na watu wenye ujuzi wa lugha: Hii husaidia kujifunza lafudhi na matumizi sahihi ya maneno.
(iv) Kutumia kamusi: Kamusi husaidia kufahamu maana sahihi ya maneno na matumizi yake.
(v) Kusikiliza na kutazama vyombo vya habari: Habari zinaongeza maarifa kuhusu lugha ya mazungumzo na maandishi.

3. Kwa kutumia mifano, fafanua dhana zifuatazo:

(i) Utata katika lugha: Hii ni hali ambapo neno au sentensi linaweza kuwa na maana zaidi ya moja. Mfano: "Ninapenda keki za mama" inaweza kumaanisha kupenda keki zinazotengenezwa na mama au keki aina ya "mama."

(ii) Rejesta: Hii ni mtindo wa lugha unaotumiwa katika muktadha maalum. Mfano: Rejesta ya kimatibabu ina maneno kama "upasuaji," "daktari," na "uambukizo."

(iii) Simo (misimu): Haya ni maneno ya mtaani au lugha ya siri inayotumiwa na kikundi fulani. Mfano: "Bize" likimaanisha kazi nyingi, au "mzigo" likimaanisha kazi ya shule.

(iv) Umahiri wa lugha: Ni uwezo wa kutumia lugha kwa usahihi, ufasaha, na kwa njia inayofaa katika muktadha wowote. Mfano: Kuweza kuandika insha yenye mtiririko mzuri wa mawazo kwa lugha ya Kiswahili.

4. Bainisha dhima ya kila mofimu iliyopigiwa mstari katika maneno yafuatayo:
(i) Mkimbizi
- M-: Inaonyesha ngeli ya nomino inayorejelea mtu mmoja, nafanya tatu umoja

(ii) Hunung'unika
- Hu-: Inaonyesha hali ya mazoea au kitendo kinachorudiwa mara kwa mara.

(iii) Asiyeridhika
- -ye-: Inaonyesha kiambishi cha urejeshi wa mtenda (kiima) anbaye ni nafasi ya tatu umoja

(iv) Watembeao
- -o: Inaonyesha kiambishi cha urejeshi wa mtenda (kiima) katika hali ya kuendeleza kitendo.
(v) Amenialika
- -ni-: Inaonyesha kiambishi kiwakilishi cha mtendwa au mtendewa (shamirisho) wa nafsi ya kwanza umoja.

(vi) Nimekufikia
- Ni-: Inaonyesha nafsi ya kwanza umoja (mimi).

(vii) Tumejitakia
- -ji-: Inaonyesha kiambishi cha kujirejea (kujitendea).

(viii) Watamfurahisha
- -m-: Inaonyesha kiambishi kiwakilishi cha mtendwa au mtendewa (shamirisho) wa nafsi ya tatu umoja.

(ix) Pangua
- -ua: Inaonyesha kitendo Cha kutendea

5. Jina lako ni Malingumu Sulubu S.L.P 1000 Magu. Andika barua ya kukiri kupokea bidhaa ulizoagiza toka kampuni ya Mchumi Traders wa S.L.P 750 Mwanza.

Malingumu Sulubu
S.L.P 1000,
Magu,
20 Januari 2025.

Meneja,
Mchumi Traders,
S.L.P 750,
Mwanza.

Yah: Kukiri Kupokea Bidhaa

Ndugu Meneja,

Ninayo furaha kukujulisha kuwa nimepokea bidhaa nilizoagiza kutoka kampuni yako. Bidhaa zilizopokelewa ni:

1. Jozi 50 za viatu vya ngozi
2. Jozi 100 za soski nyeupe
3. Dazeni 100 za penseli
4. Katoni 100 za sabuni ya mbuni
5. Seti 150 za vikombe vya plastiki

Nakushukuru kwa huduma bora na usafirishaji wa haraka wa bidhaa hizi. Naahidi kuendelea kushirikiana na kampuni yako kwa manunuzi ya baadaye.

Wako kwa dhati,
Malingumu Sulubu.


Find this and other free resources at: http://maktaba.tetea.org

***Prepared by: Maria Marco for TETEA***

6. Kwa kutumia hoja sita, fafanua mchango wa serikali katika kukuza Kiswahili nchini Tanzania baada ya uhuru.

(i) Kiswahili kama lugha ya taifa: Serikali ilitangaza Kiswahili kuwa lugha ya taifa mwaka 1967, hatua iliyosaidia kukuza matumizi yake rasmi.

(ii) Kiswahili kama lugha ya kufundishia: Kiswahili kilianza kutumiwa kama lugha ya kufundishia katika shule za msingi nchini, hivyo kuongeza usambazaji wake kwa vizazi vipya.

(iii) Kuanzisha taasisi za Kiswahili: Serikali iliunda taasisi kama BAKITA na BAKIZA kwa lengo la kukuza na kuendeleza Kiswahili.

(iv) Kutangaza Kiswahili kimataifa: Kupitia ushirikiano wa kimataifa, serikali imekuwa mstari wa mbele kushawishi matumizi ya Kiswahili kama lugha ya mawasiliano barani Afrika na ulimwenguni.

(v) Kuandaa na kufanikisha Siku ya Kiswahili Duniani: Serikali imekuwa ikihamasisha maadhimisho haya tangu UNESCO ilipotangaza Julai 7 kuwa Siku ya Kiswahili.

(vi) Kukuza fasihi ya Kiswahili: Serikali inahamasisha uandishi wa vitabu na tamthilia katika Kiswahili kupitia mashindano na utoaji wa ruzuku kwa waandishi wa Kiswahili.
7. Kwa kutumia hoja tatu, jadili dai kuwa asili ya Kiswahili ni Kiarabu kisha tumia hoja tatu kuonyesha udhaifu wa dai hilo.

Dai kuwa asili ya Kiswahili ni Kiarabu:
(i) Kiswahili kina maneno mengi yenye asili ya Kiarabu, kama vile "kitabu," "meza," na "kalamu."
(ii) Wafanyabiashara wa Kiarabu walihusika katika kuenea kwa Kiswahili kupitia pwani ya Afrika Mashariki.
(iii) Kiswahili kinatumia herufi za Kiarabu katika maandishi yake ya awali.

Udhaifu wa dai hilo:
(i) Kiswahili kina asili kubwa ya Kibantu, hasa katika sarufi na maneno mengi ya msingi kama "mama," "baba," na "ndugu."
(ii) Historia inaonyesha Kiswahili kilikuwepo kabla ya ujio wa Waarabu, na kilikuwa kimeenea kati ya jamii za Kibantu.
(iii) Licha ya maneno ya Kiarabu, Kiswahili hakitumi miundo ya kisarufi ya Kiarabu.

8. (a) Taja tofauti tano zilizopo kati ya tafsiri ya kimawasiliano na tafsiri ya kisemantiki.

(i) Tafsiri ya kimawasiliano inalenga kufikisha ujumbe kwa njia rahisi, huku tafsiri ya kisemantiki ikilenga maana halisi ya maneno.
(ii) Tafsiri ya kimawasiliano hujikita katika muktadha wa msomaji, wakati tafsiri ya kisemantiki hujikita katika lugha chanzi.


Find this and other free resources at: http://maktaba.tetea.org

***Prepared by: Maria Marco for TETEA***

(iii) Tafsiri ya kimawasiliano inaruhusu ubunifu zaidi, ilhali tafsiri ya kisemantiki ni sahihi na yenye ukali wa maneno.
(iv) Tafsiri ya kimawasiliano hufaa kwa hadhira tofauti, wakati tafsiri ya kisemantiki hufaa kwa wataalamu wa lugha.
(v) Tafsiri ya kimawasiliano inaweza kupotosha maana ya msingi, lakini tafsiri ya kisemantiki huzuia kupotosha ujumbe.

(b) Tafsiri sentensi zifuatazo katika lugha ya Kiingereza kwa kuzingatia tafsiri ya kisemantiki:

(i) Zawadi anacheza netiboli/mpira wa pete.
Zawadi plays netball.

(ii) Mama huenda sokoni kila jumamosi/kila jumamosi mama huenda sokoni.
Mother goes to the market every Saturday.

(iii) Anajua chanzo cha maradhi yake/ugonjwa wake.
He knows the source of his illness/disease.

(iv) Shangazi yangu/mama mdogo wangu atapika chapati tamu.
My aunt will cook delicious chapati.

(v) Ninapendelea/ninapenda kusoma riwaya za Kiswahili.
I prefer/I love reading Kiswahili novels.

(vi) Walimu wanafanya kazi nzuri sana.
Teachers are doing a very good job.

(vii) Mkutano wa wiki tatu/majuma matatu unakwisha/utakwisha/utafungwa leo.
The three-week meeting ends/will end/will be closed today.

(viii) Kama watashinda watapewa zawadi/tuzo.
If they win, they will be given a prize/reward.

(ix) Ulisikia lakini hukutaka kujibu/kuitika.
You heard but did not want to respond/answer.

(x) Usiende, labda kama una/labda uwe na sababu ya msingi.
Do not go, unless you have/unless there is a valid reason.


Find this and other free resources at: http://maktaba.tetea.org

***Prepared by: Maria Marco for TETEA***